

SIAN BERRY LONDON

# CHAGUA GREEN MNAMO MEI 6

## SIAN BERRY - MEYA WA LONDON

## GREENS KUKUWAKILISHA KWENYE BUNGE LA LONDON

# LONDON INAHITAJI MWANZO MPYA

**"London inaweza kuwa jiji la kijani zaidi ulimwenguni, jiji lililojiandaa vyema kwa siku zijazo. Na tunaweza kufikia azimio hilo tukiwa na Meya mpya wa Chama cha Green."**

Hivi sasa, wakazi wa London wanatamani mwanzo mpya. Ahueni inayomwinua kila mtu na kuleta mustakabali ulio salama. Ule tunaoweza kuurithisha kwa kujivunia kwa kizazi kijacho.

Sian Berry na Caroline Russell wamefanya kazi kila siku kwa miaka mitano iliyopita wakikuwakilisha wewe kama Wabunge wa Chama cha Green kwenye Bunge la London.

Hata kabla ya janga hili, kazi yao na raia na wanaharakati ilifichua matatizo makubwa.

Wapangaji wetu wamekata tamaa, ukosefu wa makazi unaongezeka, msongamano wa magari unaongezeka, na wanawake na makundi ya walio wachache wanaumizwa kila siku kwa ubaguzi na mfumo wa makosa ya jinai. Watu wa kipato cha chini wanasumbuka, na huduma zetu za vijana zinaathiriwa na kupunguziwa bajeti.

Virusi vya Korona vimefichua mapungufu mabaya zaidi katika mifumo yetu. Lakini mifumo hii inaweza kubadilishwa.

Mambo yanaweza kuwa tofauti, na wagombea wako wa Umeya na Ubunge kwa tiketi ya Chama cha Green wana mipango ya kubadilisha London.

# SERA KUU ZA CHAMA CHA GREEN

**Sera zetu kuhusu London zinaungwa mkono na watu wote katika jiji.**

## WAJIBU WA KUHESHIMU HAKI ZA KILA MTU

**Greens watasaidia kila mtu kuishi maisha yake bila ubaguzi. Tutafanya mambo yafuatayo:**

- Tutatetea uhuru wa kwenda sehemu mbalimbali, haki za raia wa EU, na kupigania kukomesha sera zote za mazingira zenye uhasama zinazolenga wahamiaji na wakimbizi.
- Tutaanzisha jitihada katika jiji zima kumaliza ubaguzi wa rangi na jinsia, kuunga mkono haki za LGBTIQA (mashoga na wasagaji), vijana na wazee wa London, na kuondoa vizuizi vinavyowakabili walemavu wa London.
- Tutalinda uhuru wa raia kwa kudhibiti mamlaka ya polisi, kuwafanya wawajibike, kukomesha utumiaji wa utambuzi wa uso, na kukomesha kuongezeka kwa visa vya kusimamishwa na kupekuliwa na polisi.

## DHIMA YA KUFANYA MAGEUZI YA UCHUMI WETU

**Meya wa Green ndiye chaguo pekee kwa ahueni halisi ya kijani. Tutafanya mambo yafuatayo:**

- Tutakuwa mabingwa wa mitaa yetu maarufu na biashara ndogo, tukijenga uthabiti kupitia kodi nafuu.
- Tutatengeneza ajira zinazozingatia mazingira ili, kutengeneza, kutumia tena na kukarabati zaidi bidhaa na huduma tunazohitaji hapa.
- Tutasaidia wafanyakazi kupitia mpango mpya wa London Living Wage kwa kiwango cha Pauni 14 kwa saa na viwango rahisi na vyepesi ambavyo waajiriwa wanaweza kukidhi.
- Tutafungua fursa kwa vijana kupitia majaribio ya Creative Autonomy Allowance - kipato cha mara kwa mara cha kusaidia kuzindua ajira katika biashara na sanaa.




## AHADI YA KUSHIRIKI MAMLAKA YANGU

**Greens wanaamini katika kuweka mamlaka mikononi mwa watu. Tutafanya mambo yafuatayo:**

- Tutazingatia ushauri wa watu tofauti tofauti katika kufanya maamuzi, kwa hivyo watu wengi wa London watakuwa na uwezo halisi juu ya sera zinazowaathiri, pamoja na bajeti ya Meya.
- Tutafanya jitihada zaidi kupata mamlaka kutoka kwa Serikali ili kuwa na usemi wa moja kwa moja juu ya kodi, NHS, makosa ya jinai, sera za makazi na mazingira - kama ilivyo huko Scotland na Wales.

## JITIHADA KWA AJILI YA MJI SALAMA NA UNAOZINGATIA AFYA

**Lengo letu ni kuhakikisha kila mtu yuko salama katika mji wetu, bila madhara yoyote. Tutafanya mambo yafuatayo:**

- Tutaweka malengo wazi ya kuzuia vurugu na kukomesha mauaji, tutawekeza katika kinga halisi kukomesha unyanyasaji dhidi ya wanawake, na huduma kwa vijana ambazo zinawasaidia kufanikiwa.
- Tutafanya jitihada zaidi kusaidia katika afya nzuri ya akili, kuifanya iwe sawa na afya ya mwili kwa umuhimu. Tutafungua maeneo zaidi ya kijani na kusaidia wakazi wa London kuungana wao kwa wao katika jumuiya zao.
- Tutafanya barabara ziwe salama kweli, kwa kuondoa vidhibiti mwendo kasi na kuwekeza katika doria ya barabarani.
- Tutafikia lengo la kuwa na hewa safi, na ukanda wenye kiwango kidogo cha hewa chafu kote jijini London, na kujitahidi kupunguza msongamano wa magari na kuwekeza kwenye mabasi yanayozingatia mazingira.




## TUTAUNDA JIJI LA KIJANI ZAIDI ULIMWENGUNI

**Meya wa Green pekee ndiye anayeweza kuaminiwa na maisha yetu ya baadaye. Tutafanya mambo yafuatayo:**

- Tutaweka malengo sahihi ya kutatua hali ya hewa na dharura ya ikolojia kabla ya mwaka 2030, na kufanya kazi na raia wetu wote kuifanikisha.
- Tutalinda maeneo ya kijani, na kuacha kutumia dawa za kuua wadudu, tutaboresha misitu na maeneo yenye maji kote jijini, na kutengeneza hifadhi mpya za mjini na mitaa ya kijani.
- Tutawekeza zaidi katika nishati mbadala na ajira mpya, na nyumba zenye mfumo wa joto na fungu jipya la fedha za kupunguza umaskini wa nishati.

## MPANGO WA WAZI WA KUIWEZESHA LONDON KUSONGA MBELE

**Greens wanataka iwe rahisi kwa kila mtu kufanya mizunguko yake. Tutafanya mambo yafuatayo:**

- Tutapunguza msongamano wa magari na kusitisha matumizi ya Silvertown Road Tunnel, na badala yake kuwekeza katika mitaa salama, sehemu za watembea kwa miguu, waendesha baiskeli, mabasi bora na njia za usafiri wa umma.
- Tutafanya nauli kuwa sawa na kutengeneza ukanda mmoja wa handaki na reli, kama vile tulivyofanya kwenye mabasi, kusaidia kila mtu aliye nje ya London kulipa kidogo kwa safari.
- Tutaongeza uwekezaji katika barabara nzuri, zisizo na msongamano wa magari, kwa ajili ya mitaa tulivu, salama, na iliyounganishwa zaidi.



# MAWAZO MAPYA KWA AJILI YA MAKAZI

**Mawazo yetu yatasaidia kila mtu kupata nyumba nzuri na salama. Tutafanya mambo yafuatayo:**

- Tutafanya nyumba zaidi kuwa chini ya udhibiti wa watu wa London, na uwekezaji mpya kupata nyumba za wafanyakazi muhimu katika Living Rent, na usaidizi zaidi kwa makazi ya ushirika na yanayosimamiwa na jumuiya
- Tutazuia upotevu wa makazi ya halmashauri kwa kuwapa wakazi zaidi uwezo wa kupiga kura dhidi ya ubomoaji, na kuanzisha Tume ya People's Land ili kwamba watu walioko maeneo mahalia waweze kuweka mipango yao binafsi ya nyumba mpya.
- Tutazuia ukosefu wa makazi kwa kufanya kazi na wapangaji ili kuboresha haki na kufuta madeni ya kodi ya pango yaliyolimbikizwa wakati wa janga hili.
- Kodi ni kubwa sana na inafanya ukosefu wa usawa kuwa mbaya zaidi. Meya wa Green hataacha kushinikiza Serikali hadi tutakapopata uwezo wa kuweka udhibiti wa kodi London.

SIAN BERRY LONDON

# SIAN BERRY - MGOMBEA WAKO WA MEYA WA LONDON

Sian ni Mbunge wa Bunge la London na alishinda nafasi ya tatu katika uchaguzi uliopita wa Meya mnamo 2016, ambapo alishinda kura za pili za Meya kuliko mgombea mwingine yeyote.

**Sian anasema: "Nimekuwa mkazi wa London maisha yangu yote ya kazi, na kwa muda wote huo nimekuwa mpangaji binafsi. Nimeshuhudia mimi binafsi kadhia ya wenye nyumba wakorofi, mabomba mabovu na kodi kubwa ya pango."**

**"Kabla ya kuchaguliwa kwenye Bunge, nilifanya kazi na jamii kote nchini kulinda mazingira na kupata ufadhili mpya mkubwa kwa huduma bora za uchukuzi."**

**"Nimefanya mengi, na niko tayari kukuhudumia wewe na jiji letu kama Meya wako wa Green."**

**"Katika Chama cha Green kuna watu wa kawaida ambao wamekuwa wanasiasa kwa sababu tunajali sana kuhusu maeneo tunayoishi, mustakabali wetu na majirani zetu."**

**"Wananchi wetu wanatamani watu wanaoweza kuwaamini ambao watasimamia haki."**

**"Pamoja na kunifanya chaguo lako la kwanza kwa kiti cha Meya, unaweza kupiga kura kwa wagombea wetu wa Bunge wenye bidii kwenye karatasi zako zote za kura katika uchaguzi huu."**



## PIGA KURA TATU KWA SIAN BERRY NA CHAMA CHA GREEN ALHAMISI, MEI 6

BERRY, Sian
Green Party
Green Party
X

London Assembly - Local
Green Party
Green Party
X

Assembly - London-wide
Green Party
Green Party
X